Halmashauri ya Wilaya ya Ileje Mkoa wa Songwe

Taarifa ya Mapato Mwezi Oktoba,2018

2.0 MAPATO:

2.1 Vyanzo vya ndani vya Halmashauri:

Kwa mwaka wa fedha **2018/2019** Halmashauri ilikisia kukusanya mapato halisi ya ndani Tshs **903,102,500.00** na mapato ya ndani ya kisekita ni **Tshs *501,661,500.00*** na hivyo kufanya jumla ya makisio kuwa **Tsh. 1,404,764,000.00**

Kwa mwezi wa **Oktoba 2018** Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha Tshs. **52,397,547.60** ya mapato ya ndani halisi hivyo kufanya Jumla ya makusanyo kuwa Tshs **156,260,033.60** sawa na asilimia **17.3** na **Tsh 81,887,250.00** ni Jumla mapato ya ndani ya kisekta sawa na asilimia.**16.32** na hivyo kufanya makusanyo ya mapato ya ndani na ya kisekta kuwa **Tsh 238,147,283.60** sawa na asilimia **16.95** kwa mchanganuo ufuatao:-

CODES	IDARA	KIASI
500A	Utawala	10,807,397.60
502A	Fedha Utawala	806,300.00
502E	Kitengo cha biashara	9,777,600.00
505A	Mifugo na Uvuvi	688,700.00
506A	Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	5,622,900.00
511A	Ujenzi	20,000.00
512	Ardhi na Mali Asili - Utawala	9,000,000.00
512H	Misitu	15,674,650.00
	Jumla	**52,397,547.60**

Hivyo kuanzia mwezi **Julai 2018** hadi **Oktoba 2018**, Halmashauri imekusanya kiasi cha **Tsh 238,277,883.60** ikiwa ni sawa na asilimia **16.96** ya lengo la mwaka.

2.2 Ruzuku toka Serikali kuu

Halmashauri ilikisia kupokea kiasi cha **Tsh.19,799,250,076.00** ikiwa ni ruzuku ya Mishahara, Matumizi mengineyo na Miradi ya Maendeleo, kama ifuatavyo:-

NA	MAELEZO	KIASI (SHS)

1	Ruzuku ya serikali kuu Matumizi mengineyo	1,027,220,000.00
2	Miradi ya Maendeleo na Mfuko wa Wahisani	4,542,100,387.00
3	Ruzuku ya Serikali kuu (Mishahara)	13,938,416,889.00
4	TASAF III	291,512,800.00
	JUMLA	**19,799,250,076.00**

3.0 Mapokezi ya Mishahara:

Kwa mwezi wa **Oktoba 2018** Halmashauri imepokea kiasi cha**Tshs. 1,064,700,000.00** ikiwa ni ya Mishahara kwa mchanganuo ufuatao:-

CODES	IDARA	KIASI
5004	GS 2 AND ABOVE- Utawala	116,423,000.00
5006	Elimu- Utawala	26,233,000.00
5007	Elimu msingi	430,544,000.00
5008	Elimu sekondari	272,477,000.00
5010	Afya-Utawala	24,810,000.00
5011	Afya-Kinga	16,077,000.00
5012	Afya- Vituo vya afya	68,168,000.00
5013	Afya- zahanati	43,111,000.00
5014	Ujenzi	19,086,000.00
5033	Kilimo	525,000.00
5017	Maji	9,281,000.00
5031	watendaji wa kijiji	36,915,000.00
5034	Mifugo na Uvuvi	1,050,000.00
	JUMLA	**1,064,700,000**

Hivyo kuanzia mwezi **Julai 2018** hadi **Oktoba 2018**,Halmashauri imepokea kiasi cha **Tsh 4,185,177,000.00** ikiwa ni sawa na asilimia **30.3** ya lengo la mwaka.

3.1 Mapokezi ya fedha za matumizi mengineyo (oc)

Kwa mwezi wa **Oktoba 2018** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs.92,286,330.00** ikiwa ni ya fedha ya matumizi mengineyo kwa mchanganuo ufuatao:-

CODES	IDARA	KIASI
5004	Utawala	0.00
5004	Utawala GPG	0.00
5006	Elimu Msingi	0.00
5008	Elimu sekondari	207,135,000
5010	Afya	5,963,000
5014	Ujenzi	0.00
5033	Kilimo na Mifugo	0.00
5017	Maji	0.00
	JUMLA	**213,098,000.00**

Hivyo kuanzia mwezi **Julai 2018** hadi **Oktoba 2018**,Halmashauri imepokea kiasi cha **Tsh. 449,802,522.55** ikiwa ni sawa na asilimia **43.79** ya lengo la mwaka.

3.2 Mapokezi ya fedha za Miradi ya Maendeleo na Wahisani.

Kwa mwezi wa **Oktoba 2018** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs. 723,908,926.79** ikiwa ni fedha ya matumizi ya miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

NA	IDARA/KITENGO	KIASI
1	HEALTH SECTOR BUSKET FUND	74,959,400
	JUMLA	**74,959,400**

Hivyo jumla ya mapokezi ya **Julai – Oktoba 2018** ni **Tshs 947,731,126.79** sawa na asilimia **20.87** ya makisio ya lengo la mwaka.

3.0 Matumizi:

Taarifa ya Matumizi imegawanyika katika sehemu kuu mbili:

3.1 Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri.

Kwa Mwaka wa fedha **2018/2019**, Halmashauri imekisia kutumia jumla ya **Tshs. 1,404,764,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

NA	CHANZO	KIASI
1	Matumizi mengineyo mapato ya ndani halisi	541,861,500.00
2	Matumizi mengineyo mapato ya ndani ya kisekta	501,661,500.00
3	Miradi ya maendeleo	361,241,000.00
	JUMLA	**1,404,764,000.00**

Mwezi **Oktoba 2018**, Halmashauri imetumia kiasi cha Tsh **62,535,954.37** kupitia vyanzo vyake vya Ndani kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo kwa mchanganuo ufuatao:-

Mchanganuo matumizi mengineyo mapato ya ndani

CODES	IDARA	KIASI
5004	Utawala	21,290,700.00
500B	Utumishi	9,853,329.70
500C	Madiwani	27,442,073.15
502A	Fedha na Biashara	592,900.00
502B	Fedha - Ufungaji wa Mahesabu	792,000.00
515B	Ukaguzi wa Ndani	479,976.24
516A	Ugavi na Manunuzi	329,976.00
518B	Tehama	141,000.00
527A	Maendeleo ya Jamii Vijana na Ustawi	1,703,999.28
	JUMLA	**62,625,954.37**

Hivyo kuanzia mwezi **Julai 2018 Hadi Oktoba 2018** Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs 176,615,133.49** kwa matumizi mengineyo ya mapato halisi ya ndani na **Ths. 9,850,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mapato halisi ya ndani na kufanya jumla ya matumizi ya mapato halisi ya ndani **THS.176,615,133.49** ambayo ni sawa na asilimia **18.65**

3.2 Ruzuku toka Serikali kuu.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri katika matumizi ya ruzuku toka serikali kuu yamegawanyika katika sehemu zifuatazo

3.2.1 Mishahara:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwezi wa **Oktoba 2018** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs. 1,064,700,000.00** ikiwa ni ya Mishahara kwa mchanganuo ufuatao:-

CODES	IDARA	KIASI
5004	GS 2 AND ABOVE- Utawala	116,423,000.00
5006	Elimu- Utawala	26,233,000.00
5007	Elimu msingi	430,544,000.00
5008	Elimu sekondari	272,477,000.00
5010	Afya-Utawala	24,810,000.00
5011	Afya-Kinga	16,077,000.00
5012	Afya- Vituo vya afya	68,168,000.00
5013	Afya- zahanati	43,111,000.00
5014	Ujenzi	19,086,000.00
5033	Kilimo	525,000.00
5017	Maji	9,281,000.00
5031	watendaji wa kijiji	36,915,000.00
5034	Mifugo na Uvuvi	1,050,000.00
	JUMLA	**1,064,700,000**

Hivyo kuanzia mwezi **Julai 2018** hadi **Oktoba 2018** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 4,185,177,000.00** ikiwa ni sawa na asilimia **30.03** ya lengo kwa mwaka.

3.2.2 Matumizi Mengineyo (OC):

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwezi **Oktoba 2018** Halmashauri tumetumia kiasi cha **Tshs 108,279,995.76** kama ruzuku ya matumizi mengineyo kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao :-

Mchanganuo matumizi mengineyo (OC)

CODES	IDARA	KIASI
507B	Elimu Msingi	15,936,734.00

509A	Elimu Sekondari-Utawala	26,081,886.00
508A	Afya	13,283,989.52
506A	Kilimo	420,000.00
	JUMLA	**55,722,609.52**

Kuanzia **Julai 2018** hadi **Oktoba 2018** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 164,002,605.28** sawa na asilimia **11.75** ya makisio ya mwaka.

3.2.3 Miradi ya Maendeleo

Mhe, Mwenyekiti,

Kwa Mwezi **Oktoba 2018,** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 26,167,514.36** kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

NA	**MAELEZO**	**KIASI**
1	TASAF	5,154,814.36
2	NSSWP	19,144,700.00
3	Multilateral UNICEF(CHMT)	1,868,000.00
	JUMLA	**26,167,514.36**

Kuanzia **Julai 2018 hadi Oktoba 2018** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 193,081,378.72** sawa na asilimia **8.48** ya makisio yote.

Mh. Mwenyekiti.Ulinganisho wa Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 ni kama ifuatavyo:

S/N	**MAELEZO**	**KIASI TSH**
1	Salio Anzia 01/10/2018	1,002,889,967.60
2	Mapato Oktoba, 2018	1,405,154,947.60
	JUMLA	**2,408,044,915.20**
	TOA	
3	Matumizi Oktoba, 2018	1,209,216,078.25

4	**Salio ishia Tarehe 31/10/2018**	**1,198,828,836.95**

Mh.Mwenyekiti salio ishia linajumuisha fedha katika akaunti zote tisa kama ifuatavyo:

S/N	JINA LA AKAUNTI	KIASI TSH
1	Akaunti ya Vyanzo vya Ndani	10,237,125.26
2	Akaunti ya Matumizi Mengineyo (OC)	33,228,330.00
3	Akaunti ya Amana	33,675,301.81
4	Akaunti ya Maendeleo	83,209,714.43
5	Akaunti ya Mradi wa Maji	2,444,317.65
6	Akaunti ya Elimu	268,096,921.13
7	Akaunti ya Afya	765,492,809.02
8	Akaunti ya Mishahara	0
9	General Fund	2,444,317.65
	Jumla kuu la Salio hadi Oktoba 31, 2018	**1,198,828,836.95**

3.0 Mafanikio

Tumefanikiwa kuendelea na ufuatiliaji wa ushuru wa huduma kutoka kampuni ya CHINA GEO ENGINEERING CO LTD inayofanya kazi ya ujenzi wa barabara ya mpemba isongole na kulipwa bill kwa certificate ya kwanza sasa tumewatumia bill kwa ajili ya certificate ya pili.

- ✓ Tumefanikiwa kukutana na uongozi wa Mgodi wa Kabulo uchimbaji wa makaa ya mawe kijiji cha kapeta na kujua stahiki za Halmashauri kama Ushuru wa Huduma na ushuru wa usafirishaji makaa ya mawe, imeshaandaliwa bill kwa ajili ya ushuru wa huduma na
- ✓

4.0 Changamoto za mapato:

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la ukusanyaji wa mapato hasa kwa mwaka huu 2018/2019 ambapo tunakusanya wenyewe bila kutumia mawakala, Halimashauri imekutana na changamoto mbalimbali katika shughuli zake za ukusanyaji mapato kama ifuatavyo:-

1. **Kutokua na vizuizi vya Chuma au Imara pamoja na Taa:**
   Mageti yetu yote yanavizuizi vya miti ambavyo baadhi ya wafanyabiashara na magari makubwa hupita bila kusimama kukaguliwa, changamoto ya mapato inafanya ujenzi wa vizuizi bora kushindikana ambavyo

husaidia usalama na usaidizi katika ukaguzi wa magari yanayosafirisha mazao na bidhaa kutoka na kuingia Halmashauri ya wilaya ya Ileje.

2. **Wafanyabiashara kutorosha mazao**
   Kumekuwepo na tabia ya wafanyabiashara kutosha mazao nyakati za usiku kitendo kinacho pelekea Halmashauri kukosa mapato. Pamoja na kuendelea kufuatilia bado changamoto hii inazidi kutokana na kuwa biashara ya mahindi imepungua na mahindi kusafirishwa kwenda

3. **Ukosefu wa vituo vya kununulia na kuuzia mazao(mahindi)**
   Wilaya yetu haina kituo cha kuuzia mahindi kwenye shirika la hifadhi ya chakula ambapo huwalazimu kusafilisha mahindi kwenda halmashauri ya mbozi.kitendo kinachopelekea wakulima na wafanya biashara kushindwa kuunza mahindi yao na kusababisha halmashauri kukosa ushuru.

4. **Kushuka kwa bei na uhitaji ya zao la mahindi/kahawa(kubadilika kwa kiwango cha tuzo cha ushuru wa mazao(Mahindi na Kahawa)**
   Kukosekana kwa wanunuzi kumepelekea kushuka kwa bei ya zao la mahindi ambacho ni chanzo kikubwa cha mapato kwa halmashauri hivyo kupelekea kushuka kwa ushuru wa chanzo hicho.

5. Baadhi ya wafanya biashara kudaganya idadi ya mazao/Mbao waliyo beba na baadhi ya watendaji wa vijiji na kata kula njama na wafanya biashara na kutorosha mazao/mbao na kusababisha halmashauli kukosa ushuru stahiki.

6. **Kuondolewa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa kwenye bajeti.**
   Vyanzo hivyo ni kama vifuatavyo. Kodi za nyumba (kasma code 502A-140408), Mabango ya biashara na matangazo (kasma code 511-140387) na ada ya masoko ya mifugo(makanyagio) (kasma code 511-140348)

7. **Suala la siasa na maslahi binafsi kuingilia kwenye zoezi la ukusanyaji wa mapato**
   Uhalisia umejitokeza pale ambapo kodi za vibanda na kodi za majengo na hatua zilipo kuwa zikichukuliwa kwa ubadhilifu ulipokuwa ukijitokeza katika ukusanyaji wa mapato

8. **Upungufu wa mashine za kukusanyia mapato(POS)**
   Kumekuwa na upungufu wa mashine za kukusanyia mapato (POS) kwa kipindi cha mwaka 2016/2018 na 2017/2018, kumekuwa na idadi ndogo ya mashine za kukusanyia mapato ya halmashauri ikilinganishwa na maeneo yanayohitaji kukusanywa mapato. Hali hii inapelekea kukosa baadhi ya mapato ambayo yangekusanywa na halmashauri. Kwa sasa halmashauri ina jumla ya POS 50 zilizonunuliwa ambapo kati ya POS hizo 47 zinafanya kazi ya makusanyo na POS 03 zinaitaji kufanyiwa matengenezo.

5.0 Mikakati katika kukusanya mapato:

Mikakati mbalimbali katika kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama ifuatavyo;-

1. Kuendelea kutoa elimu ya ulipaji ushuru kwa walipa ushuru na hasa kuhusu kauli ya Mhe. Rais juu ya ushuru ulio ondolewa na hasa wale wanaolima na kuuza nyanya, ndizi, matunda na mboga mboga n.k.kuwa ushuru wanao tozwa katika magulio ni kwaajili ya eneo analo uzia na sii kwaajili ya mazao yake.

Lakini pia Kutoa elimu kwa taasisi nyingine kuhusu suala zima la ukusanyaji wa mapato. Halmashauli imepanga kufanya kikao cha pamoja nawadau mbalimbali wakiwemo kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya, Waheshimiwa madiwani,Wafanya biashara ili kujenga uelewa wa pamoja wa juu ya suala zima la ukusanyaji wa mapato na hatimaye kuelezana mikakati itakayopelekea kuongeza mapato ya halmashauri

2. Kuimarisha vizuizi sehemu zinazo torosha mazao hasa katika barabara kuu zinazo pitisha magari mfano geti la Mbebe, geti la Shigamba, geti la Landani(kapeta),geti la Luswiswi, geti la Mlale na geti la Sapanda na kuendeleza patrol kila siku mchana na usiku
3. Kuimarisha ukaguzi wa magari ili kubaini udanganyifu unaojitokeza juu ya idadi ya mazao/ mbao zilizo pakiwa kwenye magari.
4. Kuwabaini watendaji wadanganyifu na kuwachukulia hatua.
5. Kuongeza idadi ya masine za kukusanyia mapato (POS) ambazo zitasaidia kuongeza udhibiti wa mapato na hatimaye kuongeza mapato ya halmashauri.mpaka mwishoni mwa mwaka 2017/2018 halmashauri ilikuwa imkwisha nunua jumla ya POS 50. Hata hivyo Halmashauri imetenga bajeti kwa mwaka 2018/2019 kwaajili ya kuongezaz manunuzi ya POS 21 ili kufikia idadi ya POS 71 kisha kuimarisha na kuboresha makusanyo ya mapato na hata kuongeza udhibiti wa makusanyo ya mapato na kuendelea kuchukua hatua kwa wabadhilifu.
6. Kubuni vyanzo vingine vya mapato ambavyo halmashauri ilikuwa haikusanyi ambavyo vipo kwenye sharia mama ya fedha na kwenye sharia ndogo ya halmasauri. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 halmashauri imependekeza kukusanya kwenye vyanzo vifuatavyo:
    - Kodi ya huduma (service levy) kwa wafanya biashara
    - Vibali vya ujenzi
    - Ukaguzi wa afya
    - Ada TFDA
    - Leseni za uendeshaji wa shule binafsi
    - Malighafi za ujenzi na madini
7. Uanzishaji wa mradi wa umeme wa maporomoko ya maji katika kijiji cha bwenda. Mradi huu una uwezo wa kutoa kiasi cha Megawatt 4.7 ambao utauzwa TANESCO (mpango wa mda mrefu).

Nimeambatanisha majedwali ya mchanganuo wa mapato na matumizi

b: Taarifa ya Idara ya Maji kwa mwezi Oktoba 2018

Utangulizi

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kupitia Idara ya Maji inaendelea na jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama kwa umbali usiozidi mita 400 kama Sera ya Taifa ya Maji 2002 inavyoelekeza.
Kwa kipindi cha mwezi Oktoba, Halmashauri kupitia Idara ya maji imefanya kazi zifuatazo.

- Kuendelea na usimamizi wa ujenzi mradi wa maji Mbalula, Mabula, Mapogoro/Mangwina na Kapeta
- Kuendelea na usimamizi wa uendeshaji miradi ya maji iliyokwisha kamilika
- Kuwasilisha Mkoani kablasha la usanifu mradi wa maji Itale na chabu kwa ajili ya mapitio kabla ya kuwasilisha Wizara ya Maji kuomba kibali cha kuendelea na taratibu za manunuzi katika miradi hiyo

Mafanikio:

- Kupata kibali kutoka Mkoani kwa ajili ya kuwasilisha Wizara ya Maji kablasha la Usanifu mradi wa maji Itale ili kuomba kibali cha kuendelea na taratibu za usanifu ambapo mpaka sasa kablasha hilo limewasilishwa Wizarani

Changamoto:

- Shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji bado ni tatizo hasa kata za Ibaba na Itale
- Kusua sua kwa mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji Mapogoro/Mangwina
- Mgogoro katika chanzo cha maji kilichokuwa kimependekezwa kuhudumia kijiji cha Itale kudaiwa kuwa kiko kijiji cha Sheyo hivyo hawakubali maji hayo yapelekwe Itale
- Viongozi wa kijiji cha Sheyo kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli za kilimo kwenye chanzo cha maji kilicho pendekezwa (Sanifiwa) kuhudumia kijiji cha Itale

Jedwali lifuatalo linaonesha utekelezaji wa Miradi ya Maji katika maeneo mbalimbali Wilayani kwa mchanganuo zaidi.

JINA LA MRADI	KAZI ZILIZOKAMILIKA	KAZI ZINAZOENDELEA	MAELEZO
Mradi wa maji Mabula/ Mbalula	- Ujenzi wa vituo vya maji 12 - Kulaza mabomba - Ujenzi wa choteo la maji	- Urekebishaji wa mabomba yaliyolazwa	Matenki mawili(2) ya maji bado hayajajengwa. Mkandarasi anasubiri malipo ili aweze kuendelea na ujenzi
Mradi wa maji Mapogoro/ Mangwina	- Ujenzi wa matenki mawili (2) ya maji	- Hakuna	Mkandarasi anasubiri mabomba ambayo ameagiza kiwandani ili aweze kulaza
Mradi wa maji Itale na Chabu	- Andiko limewasilishwa wizara ya Maji kuombea kibali ili miradi iweze kutangazwa	-	-
Mradi wa Maji Kapeta	- Mradi Umekamilika kwa asilimia 100	-	Mradi unasubiri kukabidhiwa

C: Taarifa ya Hali ya Chakula Wilayani kwa mwezi Oktoba 2018

01. Utangulizi.

Hali ya chakula kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni nzuri, kutokana na sababu ya kuwa na mazao ya ziada ya vyakula kama mahindi na maharage, na kuwa na mazao mengine ya chakula kama viazi vitamu, viazi mviringo, mboga, Vitunguu, magimbi na aina mbalimbali za matunda kama vile ndizi mbivu, parachichi na matikiti maji vinapatikana sokoni. Hakuna upungufu wowote wa chakula ulioripotiwa mpaka sasa. Katika mwezi huu wa Oktoba shughuli mbali mbali za kilimo zilifanyika ni pamoja na kuandaa mashamba na kupanda mahindi kwa ukanda wa juu, kuweka dawa na kuhifadhi zao la mahindi, aidha elimu ya uhifadhi wa mazao imeendelea kutolewa kwa wakulima juu ya kujiwekea akiba ya chakula cha kutosheleza mahitaji ya familia kwa mwaka mzima.

2.0 Hali ya Hewa.

Hali ya hewa ni ya baridi kidogo wakati wa asubuhi na jioni, na wakati wa mchana kulikuwa na jua la wastani. Mvua ilinyesha kwa siku moja ya tarehe 31/10/2018.

3.0 Malengo ya Uzalishaji na Utekelezaji wa Chakula kwa mwaka 2018/2019.

S/N	**ZAO**	**MALENGO**			**UTEKELEZAJI**	
	AINA	**ENEO (Ha)**	**TANI**	**TIJA**	**ENEO**	**TANI**
	MAZAO YA CHAKULA					
1	Mahindi	25,448	101,698	4	1,027	-
2	Mpunga	1,560	7,735	5		
3	Ndizi Mbichi	4,522	63,303	14		
4	Ndizi mbivu	2,082	18,738	9		
5	Maharage	13,624	27,248	2		
6	Viazi vitamu	10,565	137,345	13		
7	Viazi mviringo	1,113	8,904	8	157	
8	Ulezi	1,308	1,308	1		
9	Muhogo	7,843	70,600	9		
10	Karanga	6,778	6,778	1		
11	Magimbi	2,600	12,800	5		
12	Mboga	364	4,284	21	22	462
13	Matunda	922	14,752	16	17	240
14	Ngano	392	348	1		
15	Njegere	175	120	1		
16	Vitunguu	122	1098	9		
17	Maembe	343	5,136	15		
18	Machungwa	34	412	12		
19	Parachichi	719	15,099	21		
20	Manansi	103	2,207	21		
21	Nyanya	67	1,340	20	11	60
	JUMLA	**80,524**	**501,253**	--	**1,234**	**762**

4.0 Hali ya chakula wilayani.

Mavuno mazuri yalipatikana na ziada ya tani 51,887 za mahindi kwa msimu wa kilimo **2017/18** kunaifanya Wilaya iwe na uhakika wa chakula kwa msimu wa kilimo **2018/19.** Hakuna upungufu wowote wa chakula ndani ya wilaya na bei za mazao sokoni kwa sasa ni za wastani na zingine ni chini ya wastani mfano ni kwa zao la mahindi na Maharage.

Jedwali Na. 1 Linaonesha hali ya uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na mahitaji ya wakazi wa wilaya.

Wakazi 2017/18	**Mahitaji (tani)**		**Uzalishaji 2017/18 (tani)**		**Ziada/Pungufu (tani)**	
	Nafaka	Mikunde	Nafaka	Mikunde	Nafaka	Mikunde
142,156	**42,648**	**14,216**	**107,531**	**28,200**	**64,883**	**13,984**

Jedwali Na. 2. Linaonesha matumizi ya chakula kufikia 31/10/2018 toka katika mahitaji halisi ya chakula ikilinganishwa na idadi ya wakazi.

Wakazi 2018/19	**MAHITAJI (Tani)**		**Matumizi ya chakula kufikia tarehe 31 Okt, 2018(Tani)**		**Salio la chakula kufikia tarehe 31 Oktoba, 2018 (Tani)**	
	Nafaka	**Mikunde**	**Nafaka**	**Mikunde**	**Nafaka**	**Mikunde**
142,156	42,648	14,216	14,216	4,738	28,432	9,478

NB:

i. Mahitaji ya chakula na uzalishaji umelengwa kwa mazao ya Mahindi, mpunga, ngano na ulezi. Mikunde ni Maharage na njegere.
ii. Ziada pia ipo kwa mazao ya jamii ya mizizi na ndizi za kupikwa.
iii. Idadi ya wakazi imekokotolewa toka sensa ya watu na makazi ya mwaka **2012** kwa ongezeko la watu kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya mipango Wilaya.

5.0 Wastani wa bei za Mazao ya Chakula mwezi Oktoba soko la Itumba ikilinganishwa na mwaka uliopita

ZAO	**KIPIMO**	**BEI ZA VYAKULA (TSH)**	
		2017	**2018**
Mahindi makavu	kilo	385/=	223

Maharage makavu	kilo	1,300/=	1,200
Mchele	kilo	2,000/=	1,800
Karanga	kilo	1,300/=	1,200
Ulezi	kilo	900/=	1,000
Viazi vitamu	kilo	400/=	500
Viazi mviringo	kilo	500/=	500
Muhogo makopa	kilo	500/=	500
Nyama ya ng`ombe	kilo	5,000/=	5,000
Maziwa mabichi	lita	1,000/=	1,000
Yai	moja	400/=	250-400
Sukari	kilo	2,800/=	2800-3,000
Mafuta ya Alizeti	Lita	3,500/=	3600-4,000
Nyanya	Fungu	150/=	200-500
Vitunguu	Fungu	450/=	500
Tangawizi	Fungu	600/=	500
Mboga ya majani	Fungu	100/=	200
Parachichi	Moja	200-500/=	200-500

NB:

Bei ya mahindi kwa sasa imeshuka toka Tsh 385 kwa kilo hadi Tsh. 223 (debe Tsh 7,000 hadi 4,000 kwa sasa) baadhi ya vyakula bei imepanda kama vile ,sukari, mafuta ya alizeti, vitunguu, viazi vitamu, Ulezi, nyanya, mboga mboga na parachichi ikilinganishwa na mwaka uliopita mwezi kama huu.

6.0 Changamoto na Ufumbuzi

6.1 Changamoto

- Bei ndogo ya zao la mahindi kutokana na soko kutokuwa la uhakika
- Ongezeko la gharama za utunzaji wa mazao ghalani kusubiri soko.

6.2 Ufumbuzi wa Changamoto

- Serikali kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula Taifa-NFRA imetupa jumla ya tani 100 kuuza katika kituo cha Vwawa Mbozi kwa mwezi Oktoba, pia wananchi wanashauriwa kuuza nje ya mipaka ya nchi pale inapobidi kwa kufuata taratibu za kiserikali.
- Wakulima wameshauriwa kutumia mifuko ya PICS na njia ya mapipa ya kuhifadhia nafaka kupunguza gharama ya uhifadhi.

7.0 USHAURI ULIOTOLEWA KWA WAKULIMA

- ❖ Maafisa ugani (Kilimo) ngazi ya vijiji na kata wameendelea kutembelea wakulima na kuelekeza mbinu bora za uhifadhi mazao na ufanyaji biashara wa mazao ya nafaka pamoja na mazao ya bustani (mboga na matunda).
- ❖ Maelekezo kwa wakulima ya kutekeleza ushauri wa kuwa na bajeti ya chakula kukadiria kulingana na idadi ya watu katika kaya na kuuza ziada.
- ❖ Kufanya maandalizi ya mashamba mapema na kuandaa pembejeo.
- ❖ Udhibiti wa bungua kwenye mahindi kwa kutumia dawa kama Actellic super dust, Shumba na mifuko ya PICs na mapipa kwa uhifadhi wa mahindi na kufuata maelekezo sahihi.

D: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA YA AFYA KWA MWEZI OKTOBA 2018.

1.1 HUDUMA ZA TIBA.

Kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2018 huduma za tiba na kinga zimeendelea kutolewa katika vituo vyote 33 vya kutolea huduma za Afya.

2.1 HUDUMA YA CHANJO.

Huduma ya chanjo zimeendelea kutolewa kupitia vituo 26 vya kutolea huduma za mkoba (mobile clinic). Aidha takwimu za hali ya chanjo bado zinaendelea kukusanywa kutoka katika vituo vya tiba kulingana mwongozo wa Wizara ya Afya ambao unataka takwinu zote za afya zinatakiwa ziwe zimekusaywa kufikia tarehe 14 ya kila Mwezi na kuingiza kwenye mfumo (DHIS2) ndipo uhali wa kutumia takwimu hizo unapoanza.

AFYA YA UZAZI NA MTOTO

Huduma za Afya ya uzazi na mtoto zimeendelea kutolewa Wilayani, aidha kutokana na Idara inategemea kupata takwimu za mama Wajawazito waliojifungua kupitia mfumo wa taarifa wa Idara (DHIS2) baada ya kuingizwa kwenye mfumo huo, bado taarifa husika zinaendelea kukusanywa kutoka katika vituo vya tiba.

Aidha kwa Mwezi Oktoba hakuna kifo cha mama mjamzito kilichoripotiwa wakati ama baada ya kujifungua.

HALI YA DAWA

Kwa mwezi Oktoba, 2018 tumepokea Dawa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya kutoka Bohari Kuu ya dawa (MSD) vyenye thamani ya TZS. 19,343,000.

5.1 KUDHIBITI MAGONJWA YA KUAMBUKIZA.

Kwa kipindi cha mwezi wa Oktoba, 2018 hapakuwepo na magonjwa ya mlipuko. Aidha Idara ya Afya imeendelea kutoa elimu kwa Jamii namna ya kujikinga na ugonjwa wa EBOLA japo kwa Tanzania hakuna ugonjwa huo, lakini tahadhari zinachukuliwa kutokana ugonjwa huo kuwepo nchi Congo.

6.1 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

Kwa mwezi Oktoba, 2018 jumla ya wanachama 107 wa Mfuko wa afya wa jamii (CHF) walisajiliwa kwa jumla ya shilingi 1,070,000. Kwa mwezi Oktoba hapakuwepo na kampeni za uhamasishaji, kwa sababu bado mpango wa kuanza kutekeleza matumizi ya bima ya afya ya Jamii iliyoboreshwa unaendelea.

7.1 HUDUMA ZA WAZEE

Kwa mwezi Oktoba, 2018 vimetengenezwa vitambulisho 53 kwa ajili ya huduma za matibabu kwa Wazee zaidi ya miaka 60 na kuendelea, ambapo Wanaume waliopewa vitambulisho ni 18 na Wanawake waliopewa vitambulisho ni 35. Wananchi wameendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa Wazee waliotimiza umri wa miaka 60 kupata vitambulisho vya msamaha wa matibabu mapema badala ya kusubiri hadi kuugua, kwa kupata vitambulisho mapema vitasaidia kupata huduma za afya kirahisi pale wanapokwenda katika vituo vya tiba.

8.1 TAARIFA ZA USTAWI WA JAMII

1. Matukio ya migogoro ya Ndoa na Usuluhishi

Kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 jumla ya kesi 5 za migogoro ya ndoa na usuluhishi zimeripotiwa katika ofisi ya ustawi wa Jamii ambapo kati ya hizo kesi 3 zimesuluhishwa na wahusika wanaendelea kuishi pamoja, kesi 2 zinaendelea kusikilizwa katika ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya.

2. Matunzo kwa Wajawazito na watoto

Kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 Kesi 5 za matunzo ya watoto zimeripotiwa katika ofisi ya ustawi wa jamii ambapo kesi 2 zimesuluhishwa na huduma zinaendelea kutolewa kwa Watoto kama zilivyokua zinatolewa awali, kesi 2 zinaelendelea katika ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya na kesi 1 imepelekwa Mahakama ya mwanzo kwa hatua zaidi za kisheria.

3.Matukio ya kesi za Unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto

Kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 jumla ya kesi 12 zimeripotiwa ambapo kesi 1 imesuluhishwa,kesi 8 zipo mahakamani mashauri bado yanaendelea,kesi 3 zipo katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya.

8.1 HALI YA UKIMWI.

UNASIHI NA UPIMAJI

Ushauri nasaha/unasihi na upimaji unaendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za Afya. Ushauri nasaha/unasihi na upimaji kwa mwezi Oktoba,2018 ilikuwa kama ifuatavyo:

WALIOPATA UNASIHI			**WALIOPIMA**			**WALIOKUWA NA MAAMBUKIZI**		
ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
504	840	1344	504	840	1344	6	28	34

TOHARA KWA WANAUME

Kampeni ya tohara kwa wanaume inaendelea kufanyika tokea ilipoanza rasmi tarehe 29 mei 2013. Kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 jumla ya wateja 26 walipata huduma ya tohara katika Hospitali ya Wilaya Itumba (Static Point of service). Zoezi hili ni endelevu na linalenga kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi.

Nawasilisha.

SILVESTER A. MGINA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
ILEJE